

## **“Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku ni Hatari kwa Afya Yako”**

### **4. Athari za Uvutaji Holela wa Bidhaa za Tumbaku**

Hakuna kiwango salama cha uvutaji wa moshi wa tumbaku. Takriban watu milioni 8 hufariki kila mwaka kutokana na kutumia tumbaku na kati yake vifo milioni 1.2 ni matokeo ya uvutaji usio wa moja kwa moja.

Kuvuta kiasi kidogo cha moshi kwa muda mfupi kunaweza kusababisha uharibifu mkubwa katika mwili wa binadamu. Taarifa za kisayansi zinaonesha kuwa kuvuta moshi wa tumbaku kunasababisha:

- Vifo
- Magonjwa
- Ulemavu
- Mimba kuharibika
- Watoto kuzaliwa na uzito mdogo.

Kwa kuzingatia madhara yaliyopo kwa watumiaji na wasiotumia bidhaa za tumbaku, kudhibiti uvutaji sehemu za umma ni suala la muhimu ili kuepusha watu wasiovuta kupata madhara kutokana na moshi na wanaovuta wapunguze au kuacha matumizi.

### **5. Onyo**

Ni kosa kisheria kutumia bidhaa za tumbaku katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:

Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),  
S.L.P 1253 Dodoma au  
77150 Dar es salaam.

Simu+255 22 2450512/2450751/2452108  
Barua pepe: [info@tmda.go.tz](mailto:info@tmda.go.tz)  
Tovuti: [www.tmda.go.tz](http://www.tmda.go.tz)

**Simu bila malipo / Simu ya bure  
0800 110 084**



**TMDA Hulinda Afya ya Jamii**



## **MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**



**UVUTAJI HOLELA  
WA BIDHAA ZA TUMBAKU NA  
MAJENGO YANAYORUHUSIWA**

## **1. Utangulizi**

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni taasisi ya Serikali ilio chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto yenyeye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Kwa lengo la kulinda afya ya jamii na kwa sababu ya kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa za tumbaku ikiwa ni pamoja na magonjwa yanayohusiana na tumbaku, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ameikasimisha TMDA jukumu la kudhibiti bidhaa za tumbaku kuititia Tangazo la Serikali Na. 360 la tarehe 30 Aprili, 2021.

## **2. Uvutaji holela wa Bidhaa za Tumbaku kwenye Maeneo ya Umma**

Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, Sura 121 imekataza uvutaji wa aina yoyote ile wa bidhaa za tumbaku kwenye maeneo ya umma ili kulinda afya ya wasiotumia bidhaa hizo. Katazo hili linahusisha bidhaa za tumbaku zinazotambulika kisheria ambazo ni sigara, siga, sigarusi, misokoto, shisha, kiko na tumbaku ya unga. Bidhaa za tumbaku zisizovutwa (smokeless tobacco products) haziruhusiwi kutumika katika maeneo na mazingira yoyote nchini Tanzania.

Kifungu cha 12 cha Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, Sura 121 kimetafsiri maeneo ya umma kama mahali ambapo inatolewa huduma ya afya, maktaba, mahali pa ibada, majengo au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mikutano ya kitamaduni na kijamii, shughuli za michezo au burudani, sehemu za

huduma ya chakula, majengo ya ofisi, vyombo vyaya usafiri wa anga, ardi au maji, mabanda ya maonesho, masoko, maduka makubwa na maeneo mengine yoyote yanayotumiwa na umma.

Vilevile, katika maeneo tajwa inaelekezwa bango lenye maneno yanayosomeka "NO SMOKING" na "HAIRUHUSIWI KUVUTA SIGARA" yawekwe na kuonekana bayana.

## **3. Maeneo yanayoruhusiwa kuvuta Bidhaa za Tumbaku**

Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku inawataka wamiliki wa maeneo ya umma kutenga vyumba au maeneo maalum ya kuvutia ili kuwalinda wasiotumia bidhaa za tumbaku.

Ujenzi na mifumo ya hewa kwenye vyumba na maeneo husika yanapaswa kuzingatia masharti ya kisheria ambayo ni -

- a. Kutozidisha 25% ya eneo la jumla la sakafu;
- b. Kutenganishwa na eneo la umma kwa ukuta na mlango wa kuingilia wenyewe maneno yanayoonekana na kusomeka "SMOKING AREA" na "SEHEMU YA KUVUTIA TUMBAKU";
- c. Kuwa na vifaa vya mfumo wa uingizaji hewa unaoruhusu moshi kwenda nje ya jengo na kutozunguka kwenye eneo lingine lolote;
- d. Mfumo wa hewa utapaswa kuwekewa

milango na kifaa cha milango kujifunga yenyewe baada ya kufunguliwa pamoja na-

- (i) feni kwa vyumba visivyo na madirisha au madirisha yanayoangalia nje;
- (ii) madirisha yaliyowekwa juu umbali wa mita 2.4 kutoka kwenye usawa wa sakafu ili kuruhusu moshi kuelekea juu na nje ya jengo badala ya usawa na kusambaa kwenye chumba; au
- (iii) vifaa vya kuelekeza moshi kutoka nje ya jengo.

e. Urefu wa chumba cha kuvutia tumbaku unapaswa kuwa siyo chini ya mita tatu kutoka kwenye dari hadi sakafuni;

f. kuainisha tahadhari za kiafya kama ilivyoelekezwa kwenye aya (b);

g. kuwekewa vifaa visivyo hamishika na vya kupambana na moto; na

h. kuwa na chumba kilichowekewa vifaa visivyo shika moto.

Aidha, Kanuni ndogo ya 7 (1) na (2) ya Kanuni za Bidhaa za Tumbaku za mwaka 2014, inawataka wamiliki wote wa majengo yanayotumiwa na watu wengi kuweka vifaa vya kubaini moshi wa tumbaku na kuweka alama zinazosomeka "THIS BUILDING IS INSTALLED WITH A SMOKE DETECTOR" na "JENGO HILI LIMEFUNGWA MITAMBO YA KUBAINI MOSHI WA TUMBAKU".